Jina _____ Nambari yako _____

Sahihi yako _____

Tarehe _____

101/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA : SAA 1 ¾

FORM 4 CLUSTER EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
MUDA : 1 ¾

MAAGIZO
(a) Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.
(b) Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobakia
(c) Kila insha isipungue maneno 400
(d) Kila insha ina alama 20

Kila mtahiniwa lazima aangalie kama kurusa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

Kijitabu hiki kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

1. Insha ya <u>lazima.</u>

   Wewe ni katibu wa Jopokazi lililoteuliwa na serikali kuchunguza ongezeko la visa vya kuvunjika kwa ndoa miongoni mwa jamii. Andika ripoti yenu.

2. Eleza hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabiliana na janga la ukame nchini.

3. Asubiriye hajuti.

4. Anza kisa kwa maneno haya:

   Mtoto aliletwa mbele yangu akiwa anatiririkwa damu usoni. Singeweza kumtambua hadi pale ……...
   ……

101/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI / AGOSTI 2011

FORM 4 CLUSTER EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA

MWONGOZA WA KUSAHIHISHA

SWALI LA KWANZA
MTINDO

- Hii ni ripoti rasmi
- Sura ya ripoti izingatie haya:

(a) Kichwa – ripoti inahusu nini?
(b) Utangulizi uwe na majina ya wanajopo
(c) Uchunguzi kuwasilishwa kwa njia ya vichwa vidogo vidogo
(d) Mapendekezo yaorodheshwe kwa njia ya tarakimu au kiaya
(e) Hitimisho
(f) Sehemu ya sahihi za katibu na mwenyekiti wa jopo

MAUDHUI
Baadhi ya hoja za sababu za kuvunjika kwa ndoa

- Umaskini / ufukara uliokidhiri
- Mume / mke kutokuwa mwaminifu
- Ndoa za mapema
- Ndoa za lazima
- Mmoja kutambulika kuwa na ugonjwa hatari kama vile, ukimwi au saratani.
- Utasa au ugumba
- Ulevi wa kupindukia
- Ukatili katika ndoa k.m. kupigwapigwa kwa mwanamke

Mapendekezo

- Ushauri kutolewa kwa wale wanaooana.
- Mume na mke kuishi pamoja.
- Elimu kutolewa kuhusu majukumu ya kila mmoja katika taasisi ya ndoa.
- Sheria kubuniwa ya kurasimisha ndoa zote ili kuwa vigumu watu waliooana kuachana ovyoovyo.
- Wanaokiuka haki za wenzao katika ndoa kukabiliwa kisheria.

Tanabahi: Mtahiniwa aliyekosa kutoa mapendekezo, amepungukiwa kimaudhui.

Kijitabu hiki kina kurasa 5 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

SWALI LA PILI

Hatua za serikali katika kukabiliana na ukame. Baadhi ya hoja:

- Serikali inajenga mabwawa ya maji katika sehemu kame ili kuhifadhi maji wakati wa mvua.
- Mabwawa ya maji yaliyoko yanafanyiwa ukarabati.
- Serikali hununua mifugo kutoka kwa wafugaji wakati wa kiagazi.
- Kuna mikakati ya kuhimiza watu kutumia teknolojia ya kunyunyizia mimea maji.
- Sehemu za chemichemi za maji zinahifadhiwa.
- Serikali imepiga marufuku ukataji wa miti ovyoovyo.
- Wakulima wahimizwa kupanda mbegu maalumu zinazostahimili ukame.

SWALI LA TATU

Hii ni methali.

Maana: Mtu mwenye subira huepuka dhiki na hivyo basi hajuti baadaye.

Mtahiniwa sharti aandike kisa au visa kuthibitisha ukweli wa methali.

Tanabahi: Mtahiniwa atakayeandika kisa kisichokuwa na uhusiano na methali atakuwa amejitungia swali. Alama zake zisizidi 2. (Kiwango cha D-)

SWALI LA NNE

Mtahiniwa aanze insha kwa maneno aliyopewa. Kisa chake kihusishe:

- Chanzo cha kuvuja damu.
- Uhusiano wa mwathiriwa na msimulizi.
- Usaidizi aliopewa mwathiriwa.
- Hatima ya tukio hilo.

Tanabahi: Mtahiniwa aliyeanza kisa kwa maneno tofauti, atakuwa amejitungia swali lake. Kiwango chake ni D- (1 au 2)

MAELEZO YA JUMLA

1. Isha yoyote isiyotimiza urefu, mtahiniwa apoteze alama 2 (urefu) baada ya kutuzwa.
2. Insha isiyozingatia sura, mtahiniwa aadhibiwe alama 4 (sura) baada ya kutuzwa.
3. Mtahiniwa aliyejibu maswali zaidi ya mawili, swali la kwanza lisahihishwe na lingine moja linalotangulia pekee.

MWONGOZO WA KUDUMU

USAHIHISHAJI

Karatasi hii imedhamiria kutahini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha_ujumbe kimaandishi. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi, zenye utiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia, ubunifu mwingi, na hati nadhifu. Kutegemea maagizo ya swali lenyeywe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.

Mtahini lazima aisome insha yote ili aweze kuikadiria akizingatia viwango mbalimbali vilivyopendekezwa yaani, A, B, C ama D kutegemea mahali popote pale pafaapo.

KIWANGO CHA D
MAKI 01 – 05

1. Insha ya aina hii haileweki kwa vyovyote, ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika, uakifishaji haufai, na insha ina makosa ya kila aina ya kisarufi, kimaendelezo, kimtindo n.k.

VIWANGO TOFAUTI VYA D
D- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 01 – 02

1. Insha haina mpangilio maalum, na haieleweki kwa vyovyote vile. Kwa mfano, kunakili swali au kujitungia swali tofauti na kulijibu.
2. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili.

D **(WASTANI) MAKI 03**

1. Utiririko wa mawazo haupo.
2. Insha haieleweki.
3. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukuzwa vilivyo.
4. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
5. Hakuzingatia urefu.
6. Kuna makosa mengi ya kila aina.

D+ (KIWANGO CHA JUU) MAKI 04 – 05

1. Insha hii ina makosa mengi ya kila aina. Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kusema.
2. Insha ina lugha dhaifu ya Kiswahili na haina mpangilio.
3. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyoeleweka kikamilifu.
4. Hana uhakika wa matumizi ya lugha na hupotoka hapa na pale.
5. Mpangilio wa kazi ni hafifu hana mtiririko na hujirudiarudia.
6. Mtahiniwa ana athari za lugha ya kwanza k.m papa, badala ya baba, karamu badala ya kalamu n.k

KIWANGO CHA C
MAKI 06 – 10

Kiwango hiki kina makosa yafuatayo.
1. Mada haikukuzwa na kuendelezwa.
2. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia.
3. Hana ubunifu wa kutosha.
4. Anaakifisha sentensi vibaya.
5. Hana msamiati wa kuvutia wala msamiati mwafaka.
6. Ana makosa mengi ya hajai sarufi na msamiati.

VIWANGO TOFAUTI VYA C
C- (KIWANGO CHA CHINI|) MAKI 06-07

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha mawazo yake.
2. Hana msamiati wa kutosha wala muundo wa sentensi ufaao.
3. Mada haijakuzwa na kuendelezwa kwa njia ifaayo.
4. Ana makosa mengi ya sarufi, tahajia na msamiati.

C (WASTANI) MAKI 08

1. Anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
2. Hana ubunifu wa kutosha na dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi.
3. Uakifishaji wa sentensi zake za mzuri.
4. Amejaribu kushughulikia mada aliyopewa.
5. Ana makosa ya hijai, sarufi na msamiati.

C+ (KIWANGO CHA JUU) MAKI 09 – 10

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri lakini kwa njia isiyo na mvuto.
2. Dhana tofauti zimeanza kujitokeza kwa njia hafifu.
3. Kuna utiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo, methali na tanakali za sauti zimetumiwa kwa njia hafifu.
5. Anashughulikia mada aliyopewa kwa utiririko mzuri.
6. Kuna makosa ya sarufi, msamiati na hijai lakini insha bado inaeleweka.

KIWANGO CHA B MAKI 11 – 15

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha kuimudu lugha vilivyo.
2. Mtahiniwa anadhihilisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujieleza.
3. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
4. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha kama vile kuandika sentensi kwa njia tofauti tofauti na zikaleta maana sawa.
5. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.

VIWANGO TOFAUTI VYA B
B- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 11 – 12

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa kuonyesha hoja tofauti tofauti.
2. Kuna utiririko mzuri wa mawazo.
3. Ana uwezo wa kutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi.
4. Makosa ni machache ya hapa na pale.

B (WASTANI) MAKI 13

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Anawasilisha ujumbe waziwazi kwa mawazo yanayodhihirika.
3. Matumizi ya lugha ya mnato yamejitokeza.
4. Anatumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
5. Matumizi ya tamathali za semi yanaanza kudhihirika.
6. Makosa yanaweza kutokea hapa na pale.

B+ (KIWANGO CHA JUU) MAKI 14 – 15

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa njia inayovutia na kwa urahisi.
3. Uteuzi wake wa msamiati ni mzuri.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Uakifishaji wake ni mzuri.
6. Kuna makosa ya hapa na pale.

KIWANGO CHA A
MAKI 16 – 20

1. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato. Ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka.
2. Ana uwezo wa kutumia tamathali za lugha ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
3. Umbuji wake hudhihirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri na hali ya kumvutia msomaji wake.
4. Kazi ya mtahiniwa ni nadhifu na hati ni nzuri.
5. Insha hii imezingatia urefu unaotakikana.

VIWANGO TOFAUTI VYA A

A- (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 16-17

1. Mtahiniwa hudhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Ana utiririko mzuri wa mawazo kulingana na mada.
3. Anapamba lugha kwa kutumia tamathali za usemi.
4. Anazingatia matumizi mazuri ya msamiati na sarufi.
5. Uakifishaji wake ni mzuri zaidi.
6. Makosa machache ya hapa na pale.

A (WASTANI) MAKI 18

1. Mawazo yanadhihirika zaidi.
2. Anatumia lugha ya mnato.
3. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Anajieleza kikamilifu.
7. Makosa machache ya hapa na pale.

A+ (KIWANGO CHA JUU MAKI 1-20

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kulingana na mada.
2. Anadhihirisha mawazo yake vizuri zaidi.
3. Anajieleza kikamilifu bila shida.
4. Anatoa hoja zilizokomaa.
5. Msamiati wake ni wa hali ya juu.
6. Jumla ya makosa isizidi matano.

Jina _____ Nambari yako _____

Sahihi yako _____

Tarehe _____

101/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA : SAA 2 ½

NZAUI/MUKAA FORM 4 CLUSTER EXAMINATIONS 2011
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
MUDA : 2 ½

MAAGIZO

(a) Jibu maswali yote.
(b) Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(c) Kila mtahiniwa lazima aangalie kama kurusa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	**80**	

Kijitabu hiki kina kurasa 9 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

1. UFAHAMU:

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ni dhahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikiza mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yumkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Dar es Salaam mnamo Agosti 7, 1998 na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa "tawala – wajibika" katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingara yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na "kinyume mbele". Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauri ano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kuzipiga jeki jihudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hilo linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa malengo ya maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhali kwa utalii kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa. Kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyenginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba. Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

(a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(b) Fafanua dhana ya “kinyume – mbele” kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(d) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)

(i) Uharamia

_____

_____

(ii) Mtandao

_____

_____

(iiii) Mwambao

_____

_____

2. MUHTASARI

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Siku hiyo nilipitia mahali hapo kama yalivyokuwa mazoea yangu. Nilimuona yule mtu amelala pale pale, hatingishiki, kama nilivyokuwa nikimuona siku hizi zote, mwaka nenda mwaka rudi. Nilisimama huku nikishangaa kwa mara nyingine tena.

Nilikuwa najitayarisha kujiendea na hamsini zangu mtu huyo alipojipinda kwa mbali sana. Kwa hakika nilidhani macho yangu yananihadaa. Nikaya - kodoa zaidi ili nione vizuri zaidi ibura iliyonifunika pale. Kwa muda, hakuna lililotendeka. Nikafikisha macho yangu nikitumia nishati yote iliyomo mwilimi mwangu ili niyatoe matongo ambayo nilituhumu kwamba yalitia zingezinge nadhari yangu kiasi cha kunifanya kutoona barabara. Nilipohakikisha ya kwamba ni akili yangu tu iliyokuwa imenihadaa, nikaamua kuendelea na safari yangu kwenda kujitafutia riziki.

Hatua ya kwanza na ya pili, moyo haukunipa. Sauti katika kilindi cha moyo wangu ikanisihi na kunitafadhalisha nitazame nyuma. Jambo la kwanza nilidhani macho yangu yameingiwa na kitu kilichofanya kuona mambo yasiyokuwepo. Pili, nilidhani iwapo niliyoyaona yana msingi wowote, basi huenda ama nina wazimu, au yule mtu ni mzuka, hasa kwa vile ilionekana ni mimi tu nimuonaye. Nilikuwa niko katika hali ya kufanya uamuzi kuhusu dhana zangu hizi aina aina mtu huyo alipojingeuza, kisha akafunua macho. Moyo ulienda mbio. Nilitaka kutifua vumbi ili wazimu usinizidie lakini sikupata nafasi. Mtu yule alijizoazoa na kuketi kitako. Kisha akatokwa na maneno katika lugha iliyofanana sana na Kiswahili. Niliyaelewa aliyokuwa akisema.

Ajabu ya maajabu, mtu huyo alidai kwamba tangu alipolala kivulini hapo tangu jana baada ya chakula cha mchana, hakuota ndoto hata moja bali usingizi wake ulikuwa mithili ya gogo. Sasa nilikuwa na hakika kwamba ikiwa mimi sina wazimu, basi kiumbe yule aliyevaa ngozi iliyochakaa sana katika mpito wa miaka hakika ana wazimu. Nilitaka kuhakikisha, hivyo nilimkumbusha kwamba amelala mahali hapo kwa muda wa miaka mingi sana.

Kusikia hayo alianza kunikagua. Akasema nimevaa kizungu. Akanitajia tofauti nyingi baina ya vijana aliowazoea na mimi. Mwisho wa yote akaniuliza kama siku hiyo si tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1897. Nikadhani anafanya mzaha kwa hivyo nikacheka. Nilipoona kicheko changu kinamuudhi, nikwamwambia siku hiyo ni tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1997. Nilipoona ameshangaa kwa dhati, niligundua ukweli. Alikuwa amelala kwa karne nzima.

Maswali

(Baada ya kila swali umeachiwa nafasi unayoweza kuitumia kuandikia jibu lako kabla ya kiliandika kikamilifu).

(a) Eleza hoja sita muhimu zinazojitokeza katika aya tatu za mwanzo. (Maneno 75 – 85) (alama 6)
Utiririko (alama 2)

Matayarisho

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Jibu

(b) Kwa maneno yako mwenyewe, fupisha aya mbili za mwisho bila kubadilisha maana.
(Tumia maneno 40 – 50) (alama 5)
Utiririko (alama 2)

Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

(a) Taja na utofautishe vikwamizo vya ufizi. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(b) Tambua mzizi katika neno hili ‘mchimbaji’ . (alama 1)

_____

_____

(c) Eleza matumizi ya ‘po’ katika sentensi zifuatazo. (alama 3)

(i) Anapotembea Jane huimba _____

(ii) Atembeapo Jane huimba _____

(iii) Atembeapo Jane pana miba _____

(d) Andika kinyume cha;

Nyanya alilia na kuhuzunika katika harusi ya mama. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(e) Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha matumizi mawili tofauti ya alama hii (!). (alama 2)

(i) _____

(ii) _____

(f) Andika sentensi mbili ukitumia neno ‘mwizi’ kama (alama 2)

(i) Kivumishi _____

(ii) Nomino _____

(g) Eleza matumizi ya ‘na’ katika sentensi hii. (alama 3)

Ali na Maria wanapendana sana

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(h) Chora vielelezo matawi vya sentensi ifuatayo

Mbwa mdogo ameingia sufuriani. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

(i) Kanusha sentensi hizi. (alama 2)

(i) Wangefika nyumbani mapema wangempata mama yao angali hai.

_____

_____

(ii) Yeye akiachwa pekee ataifunga kazi.

_____

_____

(j) Geuza sentensi ifuatayo katika msemo wa taarifa.

"Nimepita kwake nyumbani lakini sikumwona ingawa ameniahidi kwamba hataondooka. Ali alituarifu." (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(k) Tumia 'O' rejeshi katika sentensi hii

Mwanafunzi ambaye amepita mtihani ni yule mwerevu. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(l) Andika katika hali ya kutendewa.

Mtoto wa waziri amekufa. (alama 2)

_____

_____

_____

(m) Unganisha kwa kiunganishi mwafaka

(i) Hataki kikombe

(ii) Hataki kisu. (alama 1)

_____

_____

_____

_____

(n) Bainisha shamrisho kipozi na kitondo katika sentensi hii.
Aliridhika na msaada aliopewa na wahisani wake. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(o) Andika ukubwa wa sentensi hii.
Nyoka aliingia ndani ya nyumba na kuacha mkia nje. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(p) Tambua aina za vitenzi katika sentensi hii.
Rehema alikuwa anataka kusoma gazeti. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(q) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi ya ngeli ya U – I. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(r) Eleza maana ya mofimu huru. (alama 1)

_____

_____

_____

_____

(s) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.
Mama alimlilia kwa dhati. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

_____

4. ISIMUJAMII

(a) Taja maneno mawili yanayounda istilahi “Isimujamii” kisha ueleze maana ya kila mojawapo. (alama 4)

(i) _____

_____

_____

_____

(ii) _____

_____

_____

_____

(b) Fafanua kaida zozote sita ambazo huathiri sajili za lugha. (lama 6)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

101/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011

NZAUI/MUKAA FORM 4 CLUSTER EXAMINATIONS 2011
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

MAJIBU

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

(a) (i) Pesa / fidia wanazolipwa maharamia.
(ii) Ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa .
(iii) Ukosefu wa utawala wa kuwajibika.

Alama 3 x 1 = 3

(b) Uharamia unaotokea barani Afrika umeelekezwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhusika mkuu wa kunusuru Afrika kutokana na njaa, magonjwa na umaskini / majanga.

Alama 1 x 2 = 2

(c) (i) Matumizi ya diplomasia na mashauriano hayafaulu katika kumaliza uharamia ulimwenguni
(ii) Matumizi ya nguvu (mashambulizi na mashtaka) yanaonekana kuendeleza uharamia.
(iii) Utawala / uongozi wa mataifa husika haujajizatiti kuuharamisha uharamia.

Alama 3 x 1 = 3

(d) (i) Maafa yanayotokana na mashambulizi ya mabomu.
(ii) Kudumaza biashara
(iii) Kuhujumu utalii wanaosafiri kwa ndege au kwa maji.
(iv) Kucheleweshwa kwa uwekaji wa nyaya / laini za kuwezesha urahisi na wepesi wa mawasiliano.
(v) Kudumaza uvuvi na shunghuli nyinginezo katika mwambao.

Alama zozote 4 x 1 = 4

(e) (i) Wizi / uvamizi / unyanganyi wa kutumia nguvu.
(ii) Mfumo wa mawasiliano yaunganishayo ulimwengu (kwa matumizi wa tarakilishi, simu au rununu)
(iii) Sehemu ya nchi iliyoko karibu na bahari / Pwani

UTUZAJI

Ondoa (i) Nusu alama kwa kila kosa la hijai litokeapo hadi la 6. ½ x 6 = 3
(ii) Nusu alama kwa kila kosa la sarufi hadi 6. ½ x 6 = 3 usitoe zaidi ya nusu alama alizozipata mwanafunzi.

Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

2. Muhtasari

(a) (i) Nipitia mahali kama mazoea yangu
(ii) Nilimwona yule mtu aliyelala pale siku zote
(iii) Nilisimama nikishangaa na nilipokuwa tayari kwenda alijipinda.
(iv) Nikakondoa macho nione vizuri lakini sikuona lolote.
(v) Nilipoanza kwenda nikaamua kutazama nyuma nikamwona akigeuka nikashtuka.
(vi) Alijigeuzageuza na kuongea lugha iliyofanana na Kiswahili nikaelewa.

1 x 6 = 6

(b) (i) Alidai alipolala tangu jana usingizi ulikuwa mithili ya gogo
(ii) Nilimkumbusha amelala hapo miaka mingi
(iii) Alinikagua akinieleza nilivaa kizungu akisema ni tarehe 10/4/1897
(iv) Nilicheka na akaudhika nikimuambia ni tarehe 10/4/1997
(v) Alishangaa nikagundua amelala karne nzima.

1 x 5 = 5
Utiririko – 4

a = 6
b = 5
ut = 4
15

Makosa ya sarufi – ½ x 6 = 3
Makosa ya hijai ½ x 6 = 3
Ziada ½ alama kwa kila maneno matano
ya kwanza kisha alama moja kwa kila maneno kumi ya ziada

3. **<u>MATUMIZI YA LUGHA</u>**

(a) t – si ghuna √ 1
d ghuna / hafifu √1

2 x 1 = 2

(b) m – chimb - aji
|
Mzizi √

(c) (i) 'Po' – ya wakati maalum
(ii) 'Po' – ya wakati wowote
(iii) 'Po' – ya mahali

(d) Nyanya <u>alicheka</u> √ na <u>kufurahi</u> √ katika harusi ya mama. Alama 2 x 1 = 2

(e) (i) Kushangaa √ alama 1
Kuamrisha √ alama 1

(f) Mvulana <u>mwizi</u>√ amekamatwa 2 x 1 = 2
<u>Mwizi</u> √ huyu ni hatari

(g) (i) Kiunganishi
(ii) Wakati uliopo
(iii) Jinsi ya kutendana / kauli ya kutendana

(h)



Jumla alama 4

(i) (i) Wasingefika nyumbani mapema wasingempata mama yao angali hai √ alama 1
(ii) Yeye asipoachwa pekee hataivuruga kazi √ alama 1

(j) Ali alituarifu kuwa alipitia kwake nyumbani lakini hakumwona ingawa alikuwa amemhahidi kuwa asingeondoka

(k) Mwanafunzi aliyepita mtihani ni yule mwerevu. √ alama 2

(l) Waziri amefiwa na mtoto wake. Alama 2

(m) Hataki kikombe wala kisu. Alama 1

(n) Msaada – kipozi √ alama 1
Wahisani - kitondo √ alama 1

(o) Joka liliingia ndani ya jumba na kuacha jikia / kia nje. Alama 2

(p) Alikuwa – TS √ Alama 1
anataka - TS √ Alama 1
kusoma – T1 √ Alama 1

(q) Kielelezo – Mti ulianguka – U √1
Miti ilianguka – I √1

(r) Hujisimia kimaana bila kupachikwa viambishi √ alama 1

(s) (i) Kwa niaba ya
(ii) Sababu ya

2 x 1 = 2

Utuzaji

(i) Ondoa alama nusu kwa kosa la hijai hadi makosa 6 x ½ = 3 alama
(ii) Ondoa alama nusu kwa kila kosa la sarufi hadi makosa 6. Kwa kila sehemu usitoe zaidi ya nusu ya alama ambazo umetuza.

4. ISIMU JAMII

(a) (i) Isimu √ – Uchangamuzi wa lugha kisayansi √1
(ii) Jamii √ - Kundi la watu √ 2 x 2 = 4

(b) Baadhi ya hoja za kuzingatiwa
- Umri
- Elimu
- Uhusiano
- Mazigira
- Mada
- Jinsia
- Mila
- Hali
- Uhusiano
- Uzoefu
- Tajiriba

n.k

Zozote 6 - kutaja ½ x 6
Kufafanua ½ x 6 Jumla 6

Utuzaji (i) Ondoa ½ alama hadi makosa 6 ya hijai ½ x 6 = 3
(ii) Ondoa ½ alama hadi makosa 6 ya sarufi ½ x 6 = 3

Jina _____ Nambari yako _____

Sahihi yako _____

Tarehe _____

101/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA : SAA 2 ½

NZAUI/MUKAA FORM 4 CLUSTER EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
MUDA : 2 ½

MAAGIZO

- Jibu maswali MANNE pekee
- Swali la kwanza ni la lazima.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.

Kila mtahiniwa lazima aangalie kama kurusa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

Kijitabu hiki kina kurasa 5 ambazo zimepigwa chapa

Geuza Ukurasa

SWALI LA KWANZA (Lazima)

KIFO KISIMANI – KITHAKA WA MBERIA

1. Msemaji A: ……. Nilikuwa nimepanga kuja kukuona leo jioni. Unasemaje?

Msemaji B: Unaichezea akili yangu.

Msemaji A : Sichezei akili yako. Wewe ndio naona kama unataka kuyachezea majaliwa yako. Unasemaje?

Msemaji B: Sijui nisemeje. Tutaongea. Tutaongea siku nyingine.

(i) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(ii) Fafanua jinsi mhusika A alivyochangia kutatiza kwa juhudi za ukombozi katika Butangi. (alama 10)
(iii) Punde tu baada ya mazungumzo haya, kunatokea nini? (alama 6)

RIWAYA

UTENGANO – S.A MOHAMMED

Jibu swali la 2 au la 3

2. Aghalabu mwanamke anajitahidi kuzorotesha ufanisi wa mwanamke mwenzake.
Jadili kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Utengano. (alam 20)

3. "Mabadiliko ni maumbile. Kutokea kwa mabadiliko ni sheria na kanuni inayoendesha ulimwengu huu …"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
(b) Taja na ufafanue mabadiliko yoyote <u>matano</u> yaliyompata msemaji.
(c) Eleza athari za mabadiliko yoyote <u>matatu</u> kati ya yale uliyotaja. (alama 6)

USHAIRI
Jibu swali la 4 au la 5

4. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuatia.

1. Maisha ya jiji ndugu, vitimbi janaa hayeshi,
Huuma ja donda ndugu, kufanya juta kuishi,
Takufanya kukosa udugu, uloenzi yako aushi,
Tahadhari mno ndugu, mikiki jiji halishi.

2. Zahama zazonga wengi, wangia kiwa wanagenzi,
Chenga kupigwa kwa wingi, kuporwa walovienzi,
Hupokwa pia mabegi, shika tama kwa majonzi,
Huapiza wao wengi, mikunguni wanyakuzi.

3. Jiji halina shirika, kila mja hamsiniza,
Bure kaka hangaika, kutaka moja himiza,
Tazomewa bure kaka, walimwengu kukuchagiza,
Jiji hili jiji gani, shirika lisohimiza.

4. La shamba jimbi sahibu, katu jijini haliwiki,
Ngoma huku sahibu, hucheza wenye mikiki,
Kitaka tata kusibu, zicheza kishamba rafiki,
Tabaki kulilia abu, takapokupata dhiki.

5. Songamano ya magari, masafu kila upande,
Konokono mwendo takiri, ilonayo madunde,
Kiwa pono e banati, singizi ambua punde,
Tajipata mashakani, kitumbua tia changa.

6. Kaditamati nafika, nanga yangu kuitia,
Ya mji kijataka, tabidi nia kutia,
Ukishikwa we tashika, haja weze kukidhia,
La sivyo utanyongeka, ubakie jililia.

Maswali

(a) Thibitisha kwamba shairi hili ni la kimapokeo. (alama 4)
(b) Bali na tarbia, tambua na utoe mifano ya bahari nyingine MBILI
zinazodhihirika katika shairi hili. (alama 2)
(c) Ni mambo gani ya mjini yanayomkera msanii? (alama 4)
(d) Tambua methali mbili zinazodokezwa katika shairi hili kwa kuziandika ki halisi. (alama 2)
(e) Taja na utoe mifano MIWILI tofauti ya idhini ya mshairi iliyotumika katika shairi hili. (alama 2)
(f) Andika ubeti wa kwanza katika lugha nathari. (alama 4)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
(i) Wanagenzi
(ii) Masafu

SWALI LA TANO

Soma shairi lifuatalo na ujibu maswali yanayofuata.

1. Yuwapi aogofyaye, ashituaye suduri,
Aje nipambane naye, kitali niko tayari,
Namtaka mimi naye, tupime nani jabari,
Jeshi hilo mtihani, Ii wapi niko imara.

2. Li wapi niko imara, siogopi nakariri,
Oktoba ni majira, ya vita hivyo kujiri,
Nami kwa silaha bora, yangu kalamu gobori,
Jeshi hilo mtihani, lije haraka nangoja.

3. Lije haraka nangoja, lije mchana dhahiri,
Li sinije kwa pamoja, kunivamia kisiri,
Vikosivye moja moja, nivitwange vi jibari,
Jeshi hilo mtihani, Ii wapi liende kapa?

4. Li wapi liende kapa, lile la kwanza hodari,
Lile la zinki na kopa, kemia lenye hatari,
Fizikia pia hapa, lijapo nilihasiri,
Jeshi hilo mtihani, lije moyo wanikera.

5. Lije moyo wanikera, lingine liso hiyari,
Lile la kushika vyura, kuvipasua vidari,
Au kulikata pera, kulichora miduari,
Jeshi hilo mtihani, lije niko makini.

6. Nalije niko makini, lile hesabu jeuri,
Lilete zake sitini, nizigeuze sifuri,
Kumi toa ishirini, ni kumi zenye dosari,
Jeshi hili mtihani, lije nipoze akili.

7. Lije nipoze akili, kurauka alfajiri,
Kigaro cha Kiswahili, nikiwashe biribiri,
Insha methali na ngeli, zote kwangu kachumbari,
Jeshi hilo mtihani, lije haraka nasihi.

8. Lije haraka nasihi, lile jeshi mashuhuri,
Lijiitalo Fasihi, la riwaya na shairi
Nilikwaruze wajihi, liogope kama ngiri,
Jeshi hili mtihani, ninalisubiri sana.

9. Nasubiri tena sana, hata liletwe kwa hori,
Uoga liache tena, wa vita kuvihari,
Tulivyokubaliana, ni Oktoba si siri,
Jeshi hilo mtihani, uwanja umeshatengwa.

10. Uwanja umeshatengwa, siku ndio nasubiri,
Ratiba ilivyopangwa, na isitie dosari,
Vita muda vilotengwa, ajizi isidhihiri,
Jeshi hilo mtihani, nalije niko imara.

11. Nalije niko imara, moyo wangu ni jasiri,
Ibaki yake kudura, ya Rabi Mola bahari,
Lije zinishe hasira, nirudi kwetu joroni,
Jeshi hilo mtihani, li wapi niko imara.

Maswali

(a) Toa kichwa mwafaka kwa shairi ulilosoma. (alama 1)
(b) Ni nini maudhui ya shairi. (alama 3)
(c) Chambua muundo wa shairi hili.
(d) Andika ubeti wa tano (5) kwa lugha ya nathari.
(e) Jadili lugha iliyotumika katika shairi hili.
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 4)
    (i) Liso shairi
    (ii) Vidari
    (iii) Jabari
    (iv) Nilihasiri

SWALI LA SITA
Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Zingine

6. HADITHI FUPI

…… alikuwa anapita kwenye ujia unaotoka kanisani akiunganisha barabara inayopita karibu na uwanja wa michezo wa Nyayo.

(a) Ni nani anayerejelewa katika maelezo haya. (alama 1)
(b) Hadithi inayohusisha haya imekolea kinaya na ubinafsi. Zidhihirisha. (alama 6)
(c) Fafanua jinsi hadithi inayorejelewa imetocheleza kaida za hadithi fupi. (alama 4)
(d) Taja mhusika wa Tabaka la juu anayehusishwa kwa mapana katika hadithi hii. (alama 1)
(e) Taja na ueleze hulka za mhusika huyo wa tabaka la juu. (alama 8)

SWALI LA SABA
FASIHI SIMULIZI

7. (a) Thibitisha dhana kuwa wimbo ni ushairi simulizi.
(b) Nyimbo zifuatazo huwa zina malengo gani ?
(i) Hadiya
(ii) Nyimbo za kisiasa
(c) Nyimbo katika Fasihi Simulizi hutambulishwa na mambo gani ?

101/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2011

NZAUI / MUKAA FORM 4 CLUSTER EXAMINATION
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SWALI LA KWANZA
KIFO KISIMANI

(i) - Msemaji A ni Zigu
- Msemaji B ni Kaloo
- Wako katika kisima cha Mkomani / Bonde la Ilangi
- Kaloo amemtembelea Zigu kwa ajili ya kutoa shukrani zake kwa Zigu na kumtuma Zigu awasilishe shukrani zake Kaloo kwa sababu ya mtoto wake kupewa kazi.

4 x 1 = 4

(ii) - Kumpa Mtemi sifa za uwongo badala ya ukweli
- Kuhudumu katika utawala mbaya
- Kuwazuia wanaharakati kuchota maji ya kisima cha Mkomani
- Kutaka kumwua Mwelusi kwa kisu
- Kumwambia Bokono kuwa aliketishwa kitini na Mungu mwenyewe na kuwa ataendelea kuongoza kwa miaka mia moja.
- Anapendekeza mfungwa Mwelusi aundiwe njama auliwe na isemekane aliuliwa na nyati au ugonjwa wa moyo gerezani.
- Kusaidia kuendeleza ufisadi wa mtoto wa Kaloo kupendelewa.

Zozote 5 x 2 = 10

(iii) - Andua anaingia akitaka kuingia kisimani achote maji / avunje kanuni
- Anaanza kubishana na Zigu kwa kukatazwa kupenya / kuingia kismani
- Mwelusi na Atega wanafika na wanajiunga na Andua kuvunja kanuni dhidi ya pingamizi za Zigu.
- Ubishi unaendelea kati ya Zigu na Mwelusi huku Zigu akiwa hamtambui Mwelusi.
- Gege anaingia na kumpongeza Mwelusi kwa kutoroka gerezani.
- Zigu hapo anamtambua Mwelusi na kutaka kumchoma kisu lakini anashauriwa na Gege asitumie kisu chake.
- Gege na Mwelusi wanaenda chemba baada ya Gege kumdanganya Mwelusi alikuwa na ujumbe muhimu.
- Kame anaingia akitaka kujua alipo Mwelusi na kukimbia akielekea walikoelekea Mwelusi na Gege.
- Sauti ya Mwelusi ya uchungu inasikika baada ya kuchomwa kisu na Gege. Mwelusi anakufa

Zozote 6 x 1 = 6

SWALI LA PILI
UTENGANO

- Kazija

  Kitendo chake kinaathiri Tamima na Maimuna.

- Mama Jeni

  - Kumtumikisha kazi chafu Maimuna na wasichana danguroni.
  - Kumfanya Dora kahaba badala ya kumlea.

- Biti Kocho

  Kumshawishi na kumtorosha Maimuna kwao aingie katika lindi la upotovu.

- Bi Farashuu

  - Kulipiza kisasi kwake kunawaathiri Tamima na Maimuna.
  - Anapinga ndoa ya Maimuna na Kabi ingawa baadaye alikubali.

- Biti Sururu

  Kitendo cha kumhifadhi Maimuna ili aendeleze ukahaba, unywaji na uuazaji wa pombe champotosha Maimuna.

- Wasichana wa danguro la Mama Jeni

  Walimwonea wivu Maimuna na kumsingizia wizi. Kitendo hicho kilimfanya Maimuna aondoke pumziko licha ya kuchafuka roho.

- Maimuna

  Anawahudumia wanaume kimapenzi na hivyo kutatiza ndoa za wanawake wengine mfano – Shoka – selume Zozote 5 x 4 = 20

  (Mtahiniwa ataje mhusika na afafanue kitendo kwa kutaja majina ya wahusika na mahali)

SWALI LA TATU

3. SWALI LA 3 - UTENGANO

(a) Muktadha

(i) Maksuudi akiwa mawazoni (akiwaza)
(ii) Muda baada ya kutoka gerezani alikotumikia kifungo cha miaka miwili.
(iii) Yuko kwake shamba (mjini hakumweki)
(iv) Anajutia tabia zake za awali ambazo zimemwathiri Zozote 4 x 1 = 4

(b) Mabadiliko

- Kupoteza kazi yake ya awali kwa sababu ya ufisadi
- Alikuwa na shamba kubwa – sasa limepungua
- Pesa zimepungua
- Amehamia mashambani
- Mpweke. Hana familia yake
- Anatangamana sasa na watu wa tabaka la chini km. Bakari na Mabruk
- Hali yake ya afya imedorora
- Ameanza juhudi za kuwasaka watu wa familia yake ambao mwanzoni aliwadharau / kuwatupa
- Ni mcha Mungu wa dhati anayeomba msamaha na kusali kwa dhati.

Zozote 5 x 2 = 10

(c) Athari za mabadiliko

(i) Hali ya afya – Unyonge wa kiwiliwili chake unabidi afanyiwe kazi / ahudumiwe hadi yake madogo kama kuwashiwa taa.
- Kulemaa mguu kunamfanya atumie bakora kujikongoja.

(ii) Upweke - Ameanzisha juhudi za kuwasaka watu wa aila yake aliowatupa awali kupitia kwa Rashid.

(iii) Ucha Mungu - Amezingatia kanuni zote za kidini kwa dhati. Anasali inavyopasa (msala u pale karibu wakati wote). Ametubia vilivyo makosa yake ya awali.

Kutaja 1 maelezo 1
Zozote 3 x 2 = 6
(Mwalimu aafiki majibu ya mwanafunzi)

SWALI LA NNE
USHAIRI

4. (a) - Limezingatia kanuni za utunzi / arudhi mashairi ya kimapokeo ndiyo yanayozingatia kanuni hizo.

Badala ya kanuni ni
- Beti sita
- Kina cha kati na cha mwisho
- Vipande viwili
- Mizani kumi na sita kila mshororo n.k

Zozote 4 x 1 =4

(b) - Mathnawi – Shairi lina vipande viwili kila mshororo ukwapi na utao.
- Ukaraguni – Vina vya kati na vile vile vya mwisho vyatofautiana ubeti hadi ubeti.

2 x 1 = 2

(c) - Kukosa undugu
- Uporaji
- Uboza wa ugeni
- Utengano wa watu mijini / ukosefu wa ushirika
- Msongamano wa magari
- Fujo 4 x 1 = 4

(d) - Jogoo wa shamba hawiki mjini (ubeti 4)
- Ukishikwa shikamana, ukiangushwa lalama 2 x 1 = 2

(e) Inkisari – Mfano ubeti 2 mshororo 2 neno walovienzi badala ya walivyovienzi
Mazida – Kaditamati badala ya kaditama ubeti 6 mshororo 1
Kubananga sarufi – Kufanya juta kuishi ubeti 1 mshororo 2
Tabdila – Neno madunde ubeti 5 mshororo 2

Zozote 2 x 1 = 2

(f) Maisha ya mjini yamejaa fujo mfululizo
Hayana urafiki wala undugu
Tahadhari uendapo huko au

Utakuja kujuta.
Maisha hayo huweza kumiza na kusumbua

Zozote 4 x 1 =4

(g) Wanagenzi – Mtu asiye na uzoefu wa jambo fulani / anayejifunza /mwanafunzi
Masafu – Misitari

5. SWALI LA TANO

(a) - Mtihani
- Niko imara / tayari
Kichwa kingine chochote kitakachoafiki maudhui ya shairi. 1 x 1 = 1

(b) Ili kufanikiwa katika jambo lolote ni lazima mtu :
- Awe tayari kwa lolote
- Awe amejiandaa vilivyo
- Awe shujaa / asiogope

(c) Muundo
(i) Kila ubeti – mistari mine (4)
(ii) Kila mstari vipande viwili (ukwapi na utao)
(iii) Kila kipande mizani 8 (mstari mizani 16)
(iv) Vina vya kati na vya mwisho
(v) Vina vya kati vinabadilika tangu ubeti mmoja hadi mwingine
Kina cha mwisho ni kile kile shairi nzima 'ri' (isipokuwa katika kibwagizo) Bahari ya Ukara
(vi) Shairi lina kibwagizo / kiitikio 5 x 1 = 5

(d) Lugha nathari
Moyo unasumbuka kungojea somo Fulani la lazima ambapo vyura hushikwa wakapasuliwa vifua.
Tunda la pera hukatwa kisha kuchorwa sura yake.
Niko tayari (nimemakinika) kupambana na mtihani

(e) Sitiari – Mtihani kuitwa jeshi
Tashihisi – Mtihani kupewa uwezo wa kupambana ka binadamu (ubeti 1 mshororo wa 3)
Utohozi – Zinki, Fizikia
Jazanda - Mtihani kufanywa dude la kuogofya
Tashbihi – Kama ngiri (ubeti 8 mshororo 3)

3 x 1 = 3

(f) (i) Liso hiyari – La lazima / upende usipende
(ii) Vidari – vifua
(iii) Jabari – Shujaa / enye uwezo / enye nguvu
(iv) Nilihasiri – Niliumize / niliharibu / nilitwange

4 x 1 = 4

SWALI LA SITA
HADITHI FUPI

6. (a) Likono 1 x 1 = 1

(b) Kinaya

- Anwani ya hadithi ni kinyume na hali halisi ya mambo hadithini
- Kizito kibambo anajiita msamaria mwema ilhali ndiye aliyemgonga Likono kwa gari lake.
- Hospitali ya Gipfel inastahili kuthamini maisha na utu lakini yathamini pesa kuliko utu.
- Daktari wa Gipfel kudai kuwa Likono alihitaji operesheni lakini Likono anapona baadaye hata bila operesheni
- Kutolipa bili kwa kutumia "Euro Card" Hospitali ya kiwango cha Gipfel yastahili kuwa na huduma ya kulipwa kwa aina zote za kadi
- Kizito kualika mgeni kwa matarajio ya kusaidia matibabu ya Likono lakini wanasaidiana kutoroka

Zozote 3 x 1 = 3

<u>Ubinafsi</u>

- Kutojali baada ya kumgonga Likono na kutaka kutoroka – Kizito anajali tu maslahi yake bali si ya majeruhi Likono
- Kizito hataki Likono aketishwe kiti cha mbele. Anataka aketi pamoja na jibwa kiti cha nyuma.
- Alijali usafi wa gari lake badala ya maslahi ya majeruhi Likono
- Kizito hakujali maslahi ya waumini alivurusha gari na kuwarushia matope wengine wakabaki kuyatema.
- Anatumia njia za kijanja kumwacha Likono hospitalini asidaiwe kulipia gharama ya matibabu.

Zozote 3 x 1 = 3

(c) - Hadithi yenyewe ni fupi (Kurasa kumi na moja) <u>Ufupi</u> wa kisa ni mojawapo ya kaida za hadithi fupi.
- Hadithi imeshughulikia <u>wazo moja</u> tu imejibana katika kisa kimoja cha Likono.
- Wahusika wake ni <u>wachache</u>
- Haina mandhari / <u>mazingira mapana</u>
- <u>Ploti yake ni sahihi</u> / haina melezo mengi

Zozote 4 x 1 = 4

(d) Kizito kibambo 1 x 1 = 1

(e) - Hana utu / katili
  - Hataki kumsaidia Likono mara anapomgonga ingawa ni yeye amemgonga kwa gari lake.
- Ni mhalifu
  - Anatumia simu akiendesha gari
  - Anataka kukimbia baada ya kusababisha ajali
  - Anakwepa kulipa bili ya hospitali
- Ana dharau
  - Kutaka Likono akae na mbwa
  - Kuwaona watu / waumini kuwa na thamani finyu kuliko gari lake.
- Ni mwongo
  - Anadanganya eti ni Msamaria Mwema
- Mwenye maringo

Zozote 4 x 2 = 8
Kutaja – 1
Maelelzo – 1

SWALI LA SABA

(a) Wimbo ni ushairi kwa sababu

(i) Wimbo, sawa na ushairi, hufuata mahadhi yenye mapigo ya muwala
(ii) Baadhi ya mashairi huimbwa mbali na kuganwa au kukaririwa.
(iii) Nyimbo hupangwa katika mafungu yaliyo sawa na beti za shairi
(iv) Mafungu ya nyimbo huwa na mistari sawa na mishororo katika ushairi
(v) Mistari ya nyimbo inayoimbwa huwa na vina au takriri inayozipa nyimbo ufululizo na sura ya shairi
(vi) Nyimbo huwa na mistari unaorudiwa mwishoni mwa kifungu (mafungu) au mazingira ya katikati mwa mafungu sawa na kibwagizo cha shairi.
(vii) Nyimbo kama shairi hutumia lugha ya mkato na teule ili kuwasilisha ujumbe kwa njia ya mvuto.
(viii) Nyimbo na ushairi hutekeleza majukumu sawa katika jamii

Zozote 6 x 1 = 6

(b) Malengo ya nyimbo

(i) Za kazi

(a) Kuwatia shime wafanyakazi
(b) Kuhimiza umoja wa wafanyakazi na jamii kwa jumla.
(c) Kuangazia haki za wafanyakazi
(d) Kutukuza bidii
(e) Kukashifu uzembe

Zozote 4 x 1 = 4

(ii) Za kisiasa

(a) Kuchochea na kuhamasisha jamii kisiasa
(b) Chombo cha kupinga ukosefu wa haki na kuwazindua watu wazipiganie
(c) Kuhimiza uzalendo
(d) Kuhimiza umoja
(e) Kuonyesha msimamo wa jamii kisiasa
(f) Kuhimiza na kuvutia wafuasi
(g) Kutaja ufanisi (kiwango) wa jamii husika

Zozote 4 x 1 = 1

(c) Mambo yanayotambulisha / pambanua muundo wa nyimbo

(i) Kugawika katika mafungu
(ii) Mafungu kugawika katika mistari (mmoja au zaidi)
(iii) Mstari kuwa na silabi / vitamkwa / mizani zenye mapigo ya kimziki
(iv) Huongozwa na mtu mmoja au wawili wanaoimba sehemu ya mstari na kupokeza waimbaji wengine.
(v) Baadhi ya nyimbo huwa na mkarara / mstari unaorudiwa rudiwa
(vi) Nafasi au uhuru wa kubuni maneno au mafungu mengine kimuktadha kwa waimbaji.
(vii) Hutumia lugha ya mkato.

Zozote 6 x 1= 6